# MNYAMA WA UFUNUO

## Sanamu, Alama na Nambari yake

***"Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, nay eye pamoja nami" Ufunuo3:20.***

## Utangulizi:

Mnyama huyu ambaye anatajwa katika kitabu cha Ufunuo ni nani? Je! tunaweza kumfahamu kwa kujifunza Biblia? Na je! tunaweza pia kuifahamu sanamu, alama na nambari yake?

Japokuwa watu wengi wamekuja wakijaribu kutoa ufafanuzi kuhusu mnyama huyu kulingana na fikira zao wenyewe; lakini Mungu ameonesha wazi katika neno lake jinsi isivyowezekana kuupata ukweli nje ya Biblia. Kwa hivyo; ikiwa wewe ni miongoni mwa wale wanaoamini katika yale ambayo biblia inayasema; na unahitaji kumfahamu mnyama huyu na maelezo yake; basi mshukuru Mungu aliyemtuma mjumbe wake Yesu Kristo, ambaye naye aliwatuma watumishi wake Manabii na Mitume ili kutupatia ufahamu. Kile utakachokisoma katika ujumbe huu ndio huo ufahamu wenyewe. Ni ufahamu wa kweli, hakika na thabiti kabisa.

## MNYAMA NI NANI?

Kwanza kabisa, fahamu na tambua kwamba neno la Mungu ni **"taa ya miguu yako, na mwanga wa njia yako",** ***soma Zaburi 119:105.*** Mjumbe wa Mungu ambaye atatufunulia huu ukweli wote pia anasema kwamba, ***"Mimi ndimi nuru ya ulimwengu, yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima" Yohana 8:12.*** Naam; Kristo ni nuru, na sauti yake ni Maandiko ya Biblia. Hii ndiyo maana Daudi anayaita maandiko kuwa ni **"taa na mwanga"** *{kwa maana nyingine ni kwamba, yanamfanya mtu kufahamu kila kitu kuhusu maisha}.* Kwa hivyo basi; hebu tusipoteze muda kwa kutazamia ufafanuzi kutoka kwingineko. Hebu na tusikilize kutoka kwa Yesu, ***"Simba wa Yuda" {soma Ufunuo 5:4-5}.*** Tega sikio tafadhali.

Wakati wa utawala ama ufalme wa Babeli ambao uliitawala dunia zamani kabla ya kuzaliwa kwa Kristo {K.K.}; mfalme wa utawala huo aliyeitwa Nebukadreza alikuwa akijaribu kufikiria moyoni mwake akitaka kujua ni kitu gani kitatokea ama kitafuata baada ya utawala wake ***{soma Danieli 2:29}.*** Na ndipo Mungu wa mbinguni alipomjulisha kwa njia ya ndoto kuhusu falme zote zitakazofuata baada yake mpaka kufikia wakati ambapo Mungu huyo wa mbinguni atakapousimamisha ufalme wake hapa duniani ***{soma Danieli 2:29-30}.*** Mungu alimjulisha mfalme Nebukadreza historia kamili ya dunia tangu wakati wake mpaka kufikia mwisho wa ulimwengu *{kwa maelezo zaidi, agiza ujumbe wetu usemao,* ***"HISTORIA YA DUNIA",*** *ili ujifunze zaidi; utatumiwa bure ujumbe huo}.*

Basi kwa maelezo hayo ambayo Mungu alimfunulia Nebukadreza; ni wazi kwamba zitakuwepo falme tano kuanzia wakati huo mpaka kufikia mwisho. **Kichwa cha dhahabu – Ufalme wa Babeli *{Danieli 2:32,36-38};* Kifua na mikono ya fedha – Ufalme wa Umedi na Uajemi *{Danieli 2:32,39; 5:31; 8:20};* Tumbo na kiuno cha shaba – Ufalme wa Ugiriki/Uyunani *{Danieli 2:32,39; 8:21};* Miguu ya chuma na nyayo zenye nusu chuma na nusu udongo – Ufalme wa Rumi *{Danieli 2:32,40-41};* Jiwe lililochongwa – Ufalme wa Mungu *{Danieli 2:34-35,44-45}.*** Hizi ndizo falme kuu za dunia kuanzia enzi ya Babeli mpaka mwisho. Ikiwa kuna falme nyingine ndogondogo; basi zinatajwa ndani ya hizi falme kuu tano tulizoziona hapa.

Nafahamu kwamba wengi wenu mmeanza kushangaa na kujiuliza, ni kwanini tunazizungumzia falme hizi, kwani zina uhusiano gani na mada yetu ya mnyama?

## MNYAMA NI MFALME {UFALME}

Wakati ufalme wa Babeli ungali ukitawala; mmoja kati ya watumwa wa Kiyahudi aliyeitwa Danieli aliota ndoto. Na katika ndoto yake, aliwaona wanyama wakubwa wanne wakitokea baharini, mmoja baada ya mwingine ***{soma Danieli 7:3}.*** Wa kwanza alikuwa kama samba ***{Danieli 7:4};*** wa pili alikuwa kama dubu ***{Danieli 7:5};*** wa tatu alikuwa kama chui mwenye vichwa vine ***{Danieli 7:6};*** na wa nne alikuwa mwenye kutisha sana, naye alikuwa na pembe kumi kichwani ***{Danieli 7:7}.*** Sasa basi; hawa wanyama ni kitu gani, wanaashiria nini hasa? Mungu wa mbinguni alimwambia Danieli kile ambacho ni jibu la swali letu akisema; ***"Wanyama hao wakubwa walio wanne ni wafalme wanne watakaotokea duniani" Danieli 7:17.***

Kabla ya kwendelea mbele zaidi; tunatoa angalizo na tahadhari kwa wasomaji wa ujumbe huu. Tafadhali hakikisha kwamba unaposoma ujumbe huu, basi uwe na biblia yako mkononi; na hii ni kwa sababu hatutaki kusikia ukizungumza habari hizi kwa kusema eti uliwasikia watu fulani wakisema, maana utakuwa unadanganya. Hapa ni Yesu Kristo mwenyewe *{na wala sio sisi}* ndiye atupaye ufunuo/ufafanuzi kuhusiana na wanyama hawa. Na hii ndiyo maana tunakupeleka hatua kwa hatua katika kufuatilia biblia ili ujumbe huu ukathibitike kuwa ni wa Kristo mwenyewe na wala si wetu sisi. Tena ili kwamba, endapo mtu atakuja na ufafanuzi ama maelezo yaliyo tofauti na haya; basi ajulikane kuwa ni mwongo, maana Mungu hana maelezo ama ufafanuzi uliotofautiana kuhusu jambo moja.

Kwa hivyo basi; Mungu mwenyewe ametuambia kwamba mnyama ni mfalme ama ufalme. Kwa vile hawa wanyama ni wafalme; na katika ndoto ya Nebukadreza tumeona falme tano zitakazotawala hapa duniani; basi ni jambo la hakika na kweli kwamba, hizi falme *{wanyama}* nne ni miongoni mwa zile falme tano za ndoto ya Nebukadreza katika Danieli 2. Kwa vile ufalme wa tano ni wa Mungu kutoka mbinguni, na huku hizi falme nyingine nne zinatokea hapa hapa duniani; basi lazima ziwe ndizo zile tulizoziona kwanza katika ndoto

*{yaani, Babeli, Umedi na Uajemi, Uyunani/Ugiriki na Rumi; linganisha* ***Danieli 7:3-7 na Danieli 2:32-33,36-41****}.* Wapo wale wanaofikiria kwamba tunajaribu kufuatilia historia kuthibitisha jambo hili la kuwafahamu wafalme ama falme hizi. Lakini ni zaidi ya hilo. Naam; ni zaidi ya historia; tunafuatilia neno la Mungu. Tafadhali sikiliza.

Mungu alimwambia Nebukadreza *{mfalme wa Babeli}* kwamba yeye ndiye kile kichwa cha dhahabu katika ile ndoto ***{Danieli 2:38}.*** Haya ni maneno ya biblia na wala si historia. Alimwambia baada yake utainuka ufalme mwingine. Tunaposoma biblia katika ***Danieli 5:30-31*** tunaona kwamba, baada ya ufalme wa Babeli kuanguka ukitawaliwa na mtoto wa Nebukadreza aliyeitwa Belshaza; kilichofuatia ni kuinuka kwa ufalme wa Umedi na Uajemi ukiongozwa na mfalme aitwaye Dario. Ufalme huu ndio unaooneshwa katika ***Danieli 8:20*** kama kondoo mwenye pembe mbili. Haya nayo ni maelezo ya biblia ni sio historia.

Baada ya ufalme wa Umedi na Uajemi, ulifuata ufalme wa Uyunani *{ama Ugiriki; ukiongozwa na Alekzanda mkuu},* ambao unaoneshwa kama beberu *{mbuzi dume}* anayeonekana akimwangusha yule kondoo ambaye ni Umedi na Uajemi ***{Danieli 8:21}.*** Baada ya hapo, unafuata ufalme wa Rumi *{linganisha* ***Danieli 8:23-24*** *na* ***Danieli 7:7-8,24-25****}.*

Basi wapendwa; haya twawaandikieni ili mtu awaye yote asitufikirie kuwa wale wahubiri wanaobahatisha unabii kwa kulinganisha na historia. Twawahubirini ujumbe utokao kwa Mungu muumba wenu kulingana ama kwa mujibu wa neno lake, yaani Biblia. Lakini kumbukeni pia kwamba, haya ni kwa wale tu watakaopewa kufahamu ***{soma 1 Wakorintho 2:6-7; Mathayo 13:11; Danieli 12:10; Luka 1:22}.***

## MNYAMA WA UFUNUO

Tayari tumeelewa vyema sasa kwamba, mnyama ni mfalme ama ufalme. Na tukaelewa vyema pia zile falme zitakazotawala katika dunia kuanzia kwa ufalme wa Babeli mpaka kuja kwa ufalme wa Mungu. Sasa je! kati ya hawa wanyama wakubwa wanne, ni yupi aliye mnyama yule atajwaye katika kitabu cha Ufunuo 13? Hebu na tumwendee Kristo ili atupe majibu sahihi, maana ni yeye pekee ndiye ajuaye ***{soma Ufunuo 5:3-5}.***

***"Kisha nikaona mnyama akitoka katika bahari, mwenye pembe kumi, na vichwa saba, na juu ya pembe zake ana vilemba kumi, na juu ya vichwa vyake majina ya makufuru. Na yule mnyama niliyemwona alikuwa mfano wa chui, na miguu yake ilikuwa kama miguu ya dubu, na kinywa chake kama kinywa cha samba, yule joka akampa nguvu zake na kiti chake cha enzi na uwezo mwingi" Ufunuo 13:1-2.***

Naam; ni yupi kati ya hao wanyama wanne tuliowaona ambaye anafanana na huyu mnyama wa Ufunuo 13? Na ikiwa huyu mnyama wa Ufunuo hafanani na hao wanyama wanne tuliowaona; na huku pia tumeona kwamba ni hizo falme nne tu ndizo zitakazotawala mpaka

kufikia mwisho na kuja kwa ufalme wa tano ambao ni wa Mungu wa mbinguni; sasa je! huyu mwingine wa Ufunuo ni yupi na anatokea wapi?

Hebu basi maandiko na yatufafanulie na kutufunulia siri hii. Katika Danieli 2, tuliona falme tano. Na katika Danieli 7, tuliona falme nne ziitwazo wanyama. Wa kwanza alikuwa kama samba; wa pili kama dubu; wa tatu kama chui mwenye vichwa vine; na wa nne ana pembe kumi kichwani. Ikiwa unafuatilia somo hili kwa umakini kabisa; basi utagundua kwamba, huyu mnyama wa ***Ufunuo 13*** ni muunganiko wa wale wanyama wanne wa ***Danieli 7:1-2;*** yaani, samba, dubu, chui na kichwa chenye pembe kumi! Sasa je! hili lina maana gani?

## MNYAMA NI MUUNGANO WA FALME ZA KIDUNIA

Falme hizi zote nne za kwanza ni falme za kidunia hii zinazoongozwa chini ya mamlaka ama utawala wa Shetani ***{****soma* ***Ufunuo 13:2,*** *alafu ulinganishe na* ***Ufunuo 19:9; Ayubu 9:24; 1 Yohana 5:19; Waefeso 2:2}.*** Hii ina maana kwamba; msingi wa hizi falme {wanyama} nne zote ni Shetani; kama vile maandiko yalivyoonesha katika ***Ufunuo 13:2*** kwamba, ***"…yule joka*** *{Shetani}* ***akampa nguvu zake na kiti chake cha enzi na uwezo mwingi".*** Tuseme nini basi?

Naam; katika Ufunuo 13, Yohana alioneshwa hizi falme zote nne zikiwa katika msingi wa Shetani *{kwa maelezo zaidi kuhusu hili, agiza ujumbe wetu usemao,* ***"SHETANI NI NANI?",*** *ili ujifunze zaidi}*. Hii ndiyo sababu zinaunganika katika mnyama mmoja *{ufalme mmoja}*. Hebu na tuelewe kwa uwazi zaidi.

Huyu mnyama wa Ufunuo 13 ana vichwa saba na pembe kumi {soma Ufunuo 13:1}. Ukiwaunganisha hawa wanyama wanne wa Danieli 7, utapata kwamba wana jumla ya vichwa saba na pembe kumi. Kwa maana kwamba; wa kwanza aliye kama samba, ana kichwa kimoja; wa pili kama dubu, kichwa kimoja; wa tatu kama chui, vichwa vinne; na wa nne, kichwa kimoja, na juu ya kichwa hicho kuna pembe kumi ***{soma Danieli7:4-8}***

Kwa hivyo basi; ukiwaunganisha wanyama hawa wanne, unapata jumla ya vichwa saba na pembe kumi. Tena utaona kwamba, maumbile *{mwonekano}* ya huyu mnyama wa Ufunuo 13, ni mkusanyiko *{umeunganisha}* wa maumbile ya hawa wanyama wanne wote wa Danieli 7. Kwa maana kwamba; mnyama wa kwanza ni kama samba – mnyama wa Ufunuo pia ana kinywa kama cha samba. Mnyama wa pili ni kama dubu – mnyama wa Ufunuo 13 pia ana miguu kama ya dubu. Mnyama wa tatu ni kama chui – kadhalika mnyama wa Ufunuo 13 pia ana mwili *{kiwiliwili}* kama wa chui. Mnyama wa nne ana pembe kumi – kadhalika mnyama wa Ufunuo 13 pia ana pembe kumi. Hii ina maana kwamba; Mungu alimwonesha Yohana zile falme ambazo hapo awali alimwonesha Danieli; lakini wakati huu akiziunganisha pamoja, maana zote zinafuata msingi mmoja wa maisha ya Shetani.

Hata hivyo, tunataka uelewe jambo fulani hapa tafadhali. Kwamba; wakati Yohana anaoneshwa haya maono; vichwa sita kati ya hivi saba vya mnyama huyu vilikuwa vimekwisha kupita, maana Yohana aliishi wakati wa utawala wa nne ambao ulikuwa ni wa Warumi na ambao ndio kile kichwa cha saba chenye pembe kumi. Kwa hivyo; ufafanuzi huu unamaanisha kwamba, mnyama wa Ufunuo 13 ni mfululizo ama mwendelezo wa hizi falme nne ambazo ni za kiulimwengu huu ***{Waefeso 2:2}***

***"Nikaona kimoja cha vichwa vyake kana kwamba kimetiwa jeraha la mauti, na pigo lake la mauti likapona. Dunia yote ikamstaajabia mnyama yule" Ufunuo 13:3.*** Tumeona kwamba; Yohana aliishi katika wakati wa utawala wa Warumi ambao ndio yule mnyama wa nne wa Danieli 7:7, na ambao ndio kile kichwa cha saba chenye pembe kumi cha Ufunuo 13. Kwa kuwa tayari hivi vichwa *{falme}* sita vilikuwa vimekwisha kupita; basi hiki kichwa ambacho Yohana alioneshwa kikipata jeraha la mauti si kingine, bali ni ufalme wa Rumi *{yaani, kichwa cha saba}*. Hata hivyo; hilo jeraha la mauti halikutokea katika wakati wa Yohana, maana Yohana alikufa kabla jeraha hilo halijatokea. Kwa hivyo je! ni lini ambapo ufalme wa Rumi *{yaani, kichwa cha saba}* ulipata jeraha la mauti? Kulingana na historia; tunafahamu kwamba ufalme wa Rumi ulianza kutawala tangu mwaka wa 31 K.K. *{yaani mwaka wa 31 kabla ya Kristo}* mpaka mwaka wa 476 B.K. *{yaani, mwaka wa 476 baada ya Kristo}*. Sasa je! ni kitu gani kilitokea katika mwaka huo wa 476 B.K.? Naam; watu wasio wa asili ya Rumi waliuvamia huo ufalme na kumuua mfalme wake aliyeitwa Romulus Augustolos katika mwaka huo. Na hivyo ndivyo ambavyo kichwa *{ufalme}* kilivyopata jeraha la mauti.

## PEMBE KUMI

Tukirudi katika ile ndoto ya mfalme Nebukadreza, tuliona miguu ya chuma ambayo ni ufalme wa Rumi ambao katika ***Danieli 7:7,*** tuliona ukiwa na pembe kumi kichwani mwake. Tuliona pia katika ***Danieli 7:8,*** pembe nyingine ndogo ikizuka kati ya zile kumi. Hii pembe ndogo ni nini? Pembe ni nini katika unabii wa biblia?

***"Na habari za zile pembe kumi, katika ufalme huo wataondoka*** *{watainuka/watatokea}* ***wafalme kumi; na mwingine ataondoka*** *{atainuka}* ***baada ya hao; naye atakuwa mbali na hao wa kwanza; naye atawashusha wafalme watatu" Danieli 7:24.***

## WAFALME {PEMBE} KUMI, NA MWINGINE MMOJA

Katika kipindi cha utawala wa kichwa hiki ambacho kilipata jeraha la mauti; mmoja wa wafalme wake aitwaye Konstantini *{Constantine}* aliamini katika ukristo wa kikatoloki na akaufanya kuwa dini ama imani inayokubalika katika ufalme wote wa Kirumi. Hapo ndipo mkuu wa kanisa la katoliki alipoanza kuinuka na kuwa na nguvu ama uwezo mwingi na hata akaanza

kuitwa kwa jina la **“PONTIFA”;** jina ambalo lilikuwa la wafalme peke yao. Katika kipindi hicho, kulitokea uasi kaskazini mwa Afrika ambako kulikuwa ni sehemu ya himaya ama utawala huo wa Rumi. Watu waliojulikana kama Wavandali katika kanda hiyo wakaasi na wakauvamia mji mkuu wa Rumi katika mwaka wa 429 B.K. Baada ya mapigano makali, hawa Wavandali walifanikiwa kuitenga sehemu hiyo kutoka katika huo ufalme katika mwaka wa 435 B.K. Baadaye waliingia katika mji wa Roma katika mwaka wa 455 B.K. na kupora mali nyingi. Maneno ya Danieli 7:8 yasemayo kwamba, “ambayo mbele yake pembe tatu katika zile za kwanza zikang’olewa kabisa”, yanathibitisha kuwa hizi pembe kumi hazikuinuka kwa pamoja, bali ziliinuka moja baada ya nyingine.

## PEMBE {FALME} TATU ZA KWANZA, NA PEMBE NDOGO

Baada ya kuivamia Roma na kujitangazia taifa lao huru; basi wakawa ndio pembe ya kwanza kati ya kumi kuinuka, na wakawa pia pigo kwa ufalme wa Kirumi na chanzo cha jeraha la mauti. Na hivyo basi; ufalme wa Kirumi ukaanza kuanguka. Hawa Wavandali hawakuwa warumi; nao walitawala katika miaka ya 429 – 548 B.K. kaskazini mwa Afrika.

Katika mwaka wa 476 B.K. uliinuka ufalme mwingine mdogo *{waliomwasi mfalme wa Rumi}* katika eneo la Italia ulioitwa Heruli {Herulis} ama Waheruli walioongozwa na Odoaka *{Odoecer}* ambaye alimuua mfalme wa mwisho wa Rumi, yaani, Romulus Augustolos, na hivyo kupeleekea kichwa cha saba na ambacho ni cha mwisho cha mnyama wa Ufunuo 13 kupata jeraha kamili la mauti.

Katika nyakati hizo, Kanisa la Kirumi chini ya uongozi wa Papa, liliinuka na nguvu ama uwezo mwingi. Kanisa hili ndilo ile pembe ndogo iliyo tofauti na zile kumi. Basi huyu kiongozi mkuu wa kanisa la Kirumi *{yaani, Papa};* akichukizwa na haya mataifa *{dola}* mawili yaliyoinuka na kujitenga na ufalme mkuu; tena ambao hawakuwa wa asili ya Rumi, na kwa kuona hatari ya hawa watu kuingilia *{kuathiri}* imani ya kanisa hilo; basi alimwomba mfalme wa mashariki aliyekuwa huko Konstantinopo *{Constantinople}* amsaidie kuwaondoa hao wavamizi *{yaani, Wavandali na Waheruli}.* Hawa Waheruli ndio pembe ya pili kati ya mumi kuinuka baada ya kufa kwa kile kichwa.

Katika mwaka wa 488 B.K. mfalme Sino wa Konstantinopo aliliunganisha jeshi lake na kundi lingine lililokuwa limeinuka katika eneo la mashariki ya ufalme wa Rumi ambalo pia lilikuwa limejitenga kutoka katika utawala huo wa Kirumi. Kundi hilo liliongozwa na mfalme aliyeitwa Theondoriki *{Theondoric},* na kundi lenyewe liliitwa Ostrogothi *{Ostrogoths}* ama Waostrogothi. Hawa nao hawakuwa wa asili ya Kirumi. Nao ndio pembe *{ufalme}* ya tatu kuinuka baada ya kuanguka kwa ufalme mkuu wa Kirumi.

Basi katika mwaka wa 493 B.K. Papa, ambaye ni mkuu wa kanisa la kikatoliki, alimuunga mkono huyu Theondoriki wa Waostrogothi *{kundi la mashariki}* na wakaliondoa

kundi la Waheruli na kumuua mfalme wake aliyeitwa Odoaka, na kuliweka eneo hilo chini ya utawala wao. Kwa hivyo; pembe ya kwanza kati ya zile tatu ikawa imeangushwa ama kung'olewa. Nao hao Waostrogothi wakaendelea kutawala Italia.

Kwa upande wa mashariki; mfalme Justiani *{Justian}* aliamua kuuimarisha ufalme wa Kirumi kwa kushirikiana na Papa. Kwa hivyo, akayatuma majeshi yake huko kaskazini mwa Afrika na kuwang'oa ama kuwaondoa hao Wavandali. Wakati majeshi ya Justiani yalipokuwa yakirudi nyumbani kutoka huko kaskazini mwa Afrika, walipitia Italia na wakaanza kupigana na Waostrogothi. Mapigano hayo yalikuwa makali sana na yalichukua muda wa miaka kumi na nane. Mwishowe walifanikiwa kuwang'oa na kuwaondoa hao Waostrogothi walioongozwa na Theondoriki.

Kwa hivyo; hizi ndizo pembe *{falme}* tatu za kwanza kuinuka kati ya zile kumi *{yaani, Wavandali, Waheruli na Waostrogothi}* baada ya kichwa cha saba kupata jeraha la mauti; na ambazo pia ziling'olewa na pembe ndogo; yaani, kanisa la Kirumi chini ya uongozi wa Papa likiwatumia hao wafalme. Sasa basi; baada ya mfalme justini kushirikiana na Papa na kuwang'oa hao watawala *{wafalme}* wasio wa asili ya Kirumi, ni kitu gani kiliendelea?

## JERAHA LA MAUTI LAPONA

Kumbukeni; Mungu alikuwa amemwambia Danieli kwamba; kutoka katika huu ufalme wa Kirumi, zitainuka falme nyingine zilizo ndogo kumi ***{soma Danieli 7:24-25}.*** Basi hizi falme ndogo zisingeweza kusimama wakati ambapo ufalme mkuu nao ungali umesimama. Na hiyo ndiyo maana katika ufunuo 13, Yohana alioneshwa hiki kichwa *{ufalme mkuu}* cha saba kikipata jeraha la mauti. Ni baada ya kuwa kimeanguka ndipo zile falme ndogo kumi zianze kuinuka. Baada ya mfalme Justini kushirikiana na Papa na kuyang'oa makundi matatu yaliyoasi *{yaani, Wavandali, Waheruli na Waostrogothi};* ambako pia ni kuangushwa ama kung'olewa kwa pembe tatu za kwanza; basi akaliunganisha tena eneo hilo lote chini ya himaya yake. Na pia akamkabidhi Papa mamlaka ya kuwa kiongozi juu ya magavana wote wa eneo la magharibi na kuliita eneo hilo kama **"ufalme wa Kirumi uliofufuka".** Katika mwaka wa 554 B.K. Justini aliapishwa na Papa kuwa mfalme wa utawala huo wote wa Kirumi uliofufuka. Na kupitia kwake, jeraha la mauti likawa limepona; naye akiwa ndiye pembe ya nne kuinuka kati ya zile kumi. Mungu alimwambia Yohana kwamba; baada ya jeraha la mauti kupona, mnyama huyu kupitia kwa pembe hizi, ataendelea kwa muda wa miezi arobaini na miwili ***{Ufunuo 13:5}.***

## KIPINDI CHA MIEZI AROBAINI NA MIWILI

Kumbukeni; katika ndoto ya mfalme Nebukadreza, tuliona falme tano pekee zikitawala kwa mfululizo katika dunia mpaka mwisho. Na tukaona ufalme wa nne ukipata jeraha la mauti

ambalo baadaye lilipona na hivyo ufalme huo ukaendelea kwa kupitia falme nyingine ndogo *{pembe kumi}* zilizoinuka. Tukaona pia jinsi ambavyo pembe nyingine ndogo *{kanisa la Kirumi/Katoliki}* ilivyoinuka na kusaidia kuziangusha pembe tatu za kwanza ***{Danieli 7:8}.*** Mfalme Justini *{ambaye ni pembe ya nne kati ya kumi kuinuka}* aliyeapishwa na Papa katika mwaka wa 554 B.K. na kuutangaza ufalme wake kama ufalme wa Kirumi uliofufuka, akafanyiza kupona kamili kwa jeraha la mauti; na ukawa pia ndio mwanzo wa kipindi cha miezi arobaini na miwili ya mnyama kuendelea kutawala kupitia kwa pembe hizi. Sasa je! kipindi hiki kitaishia lini?

Katika mwaka wa 800 B.K. Charlemage mkuu aliinuka kwa nguvu baada ya Justini kwa kuapishwa na Papa. Huyu akawa pembe ya tano kuinuka. Katika mwaka wa 962 B.K. pembe ya sita iliinuka kwa nguvu chini ya uongozi wa Otto von ambaye pia aliapishwa na Papa *{kwa maelezo zaidi; soma kitabu cha kihistoria kisemacho, "THE EUROPEAN HISTORY & THE CHURCH"}.* Baada ya Otto von katika mwaka wa 1530 aliinuka Charles V ambaye pia aliapishwa na Papa, na hivyo kuwa pembe ya saba kuinuka. Pembe ya nane ikainuka katika mwaka wa 1804, chini ya mfalme mkuu wa Ufaransa aliyeitwa Napoleon Bornapert ambaye pia aliapishwa na Papa. Huyu aliendelea kutawala mpaka mwaka wa 1814, na baada ya hapo akang'olewa na Uingereza.

Ukihesabu kuanzia kipindi cha justini *{pembe ya nne}* katika mwaka wa 554 B.K. mpaka kufikia mwaka wa 1814 B.K. ambao Napolioni aliangushwa na Uingereza, utakuta kwamba ni kipindi cha miaka 1,260. Katika unabii wa biblia, siku moja ni sawa na mwaka mmoja ***{soma Ezekieli 4:6; Hesabu 14:34}.***

Kwa kupiga mahesabu; kipindi cha miezi 42 ni sawa na siku 1,260 *{yaani, siku 30 * 42 = 1,260}* ambazo katika unabii ni sawa na miaka 1,260 *{yaani, siku 1 = na mwaka 1; siku 1,260 = na miaka 1,260}.* Kwa hivyo basi; baada ya jeraha la mauti kupona katika mwaka wa 554 B.K. mnyama huyu *{ufalme wa kirumi}* kupitia kwa hizi falme *{pembe}* ndogo, aliendelea kwa miezi 42, ambayo ni miaka 1,260, iliyoishia kwa Napolioni katika mwaka wa 1814 B.K. pembe ya nane kati ya kumi.

Katika mwaka wa 1870 B.K. Hitla wa Ujerumani aliyaunganisha majeshi yake na ya Italia yaliyokuwa chini ya Musolini, wakijaribu kuufufua huo ufalme katika kipindi chao; waliyashinda maeneo mengi ya utawala wa zamani na kuendelea kutawala mpaka mwaka wa 1945 B.K. walipoangushwa na majeshi ya Uingezera. Huo utawala wao ukawa ni pembe ya tisa kuinuka kati ya kumi. Sasa basi; imesalia pembe moja kuinuka ili kukamilisha jumla ya pembe kumi za ***Danieli 7:8,24.*** Kwa kuwa Mungu wa mbinguni hawezi kusema uongo; basi hii pembe ya kumi ni lazima iinuke na kutawala. Tangu mwaka wa 1945 B.K. hatujaona tena ufalme mwingine wa Kirumi ukiinuka kutawala. Kwa hivyo, hii pembe ya kumi bado haijainuka mpaka leo. Na hii inatupeleka kwa mnyama mwingine. Ni mnyama yupi tena?

## MNYAMA WA UFUNUO 17

***"…nikaona mwanamke, ameketi juu ya mnyama mwekundu sana,..mwenye vichwa saba na pembe kumi" Ufunuo 17:3.*** Mnyama huyu aliyembeba mwanamke ni nani? Je! anaweza kuwa ndiye yule mnyama wa Ufunuo13?

Kwa kuwa kuna falme tano pekee zitakazoinuka, na wa tano ukiwa ni ufalme wa Mungu *{lile jiwe};* ni upi kati ya hizi nne ambao ndio mnyama aliyembeba mwanamke? Wakati Danieli alipooneshwa hawa wanyama wanne, aliambiwa; ***"…yafunike maono hayo; maana ni ya wakati ujao baada ya siku nyingi" Danieli 8:26.*** Kile alichoambiwa Danieli kufunika, ndicho kile alichoambiwa Yohana kufunua; maana Mungu alimwambia Yohana kwamba, ***"Usiyatie muhuri*** *{yaani, usiyafunike}* ***maneno ya unabii wa kitabu hiki, kwa maana wakati huo umekaribia" Ufunuo 22:10.*** Nyakati za mwisho alizooneshwa Danieli ndizo wakati wa Yohana mpaka kufikia leo hii.

Kwa hivyo; si kwamba Yohana alioneshwa vitu tofauti na vile alivyooneshwa Danieli. Danieli aliishi katika enzi ya utawala wa wanyama wawili wa kwanza; yaani, katika ufalme wa Babeli na katika ufalme Umedi – Uajemi. Yohana pia aliishi katika enzi ya utawala wa mnyama wa nne *{yaani, ufalme wa Rumi}* ambaye pia ni kichwa cha saba chenye pembe kumi katika Ufunuo 13. Hata hivyo; Yohana hakuziona hizi pembe kumi zikiinuka katika siku zake, maana yeye alikufa kabla ya pembe hizi kuanza kuinuka moja baada ya nyingine. Kwa vile Yohana aliishi katika enzi ya kichwa cha saba katika Ufunuo 13 na hakumwona mwanamke akikikalia, na huku pia vichwa *{falme}* sita vikiwa vimekwisha kupita; basi inaonesha kuwa, hivi vichwa saba na pembe kumi katika Ufunuo 17, ambazo zimekaliwa na mwanamke, zilikuwa ziinuke baadaye.

Hali tukielewa vyema kwamba hakuna falme nyingine zitakazoinuka nje ya hizi falme tano, na kwamba wakati wa Yohana tayari vichwa sita vilikuwa vimekwisha kupita, na cha saba *{ufalme wa Rumi}* kilikuwepo, na vichwa hivi vyote saba havikukaliwa na mwanamke; basi ni wazi kwamba vichwa saba vya Ufunuo 17 ni pembe saba kati ya kumi zinazooneshwa katika ***Danieli 7:7 na Ufunuo 13:12.*** Hebu na tuelewe tafadhali.

## MWANAMKE

Ili kuanza habari za mnyama wa Ufunuo 17, tunahitaji kwanza kufahamu kwamba huyu mwanamke aliyemkalia mnyama huyu ni nani? Je! biblia inasema kuwa mwanamke ni nani/nini? Katika ***Ufunuo 12:1-5,*** tunasoma habari za mwanamke aliyevikwa jua, na mwezi ukiwa chini ya miguu yake. Na mwanamke huyo anaonekana akimzaa mtoto wa kiume ambaye joka alikuwa amejiandaa kummeza punde tu azaliwapo. Lakini mtoto huyo akanyakuliwa mpaka mbinguni katika kiti cha enzi cha Mungu. Baadaye, yule joka akafanya vita na uzao wa huyo mwanamke uliosalia; wale ambao wanazishika amri za Mungu na kuwa na ushuhuda wa Yesu *{soma* Ufunuo

***12:17}.*** Kwa hivyo katika biblia, Mwanamke huashiria ama kumaanisha Kanisa. Na joka ni Shetani ***{soma Ufunuo 12:9}.*** Hapa anaonekana akifanya vita na Kanisa la Mungu. Sasa je! ni kusema kwamba Kanisa la Mungu ndilo mwanamke aliyemkalia mnyama wa Ufunuo 17? Sikiliza tafadhali; ***"Nitakuambia siri ya mwanamke*** *{kahaba}* ***huyu {Ufunuo 17:7}" aketiye juu ya maji mengi {****yaani, watu wengi;* ***Ufunuo 17:15}*** pamoja naye. Kahaba yupi? ***"…nikaona mwanamke, ameketi juu ya mnyama mwekundu sana…" Ufunuo 17:3.***

Kwa vile mwanamke ni Kanisa, na yule aliye juu ya mwanamke ni kahaba; basi hawezi kuwa Kanisa la Mungu, bali yeye ni ***"…sinagogi la Shetani" Ufunuo 3:9.*** Shetani ameudanganya ulimwengu wote *{kwa maelezo ya msaada zaidi; agiza ujumbe wetu usemao,* ***"ROHO YA SABATO ZA BWANA",*** *tutakutumia bure ili ujifunze zaidi}.* Na hii ndiyo maana Wafalme wa dunia wanaonekana kulewa kwa mvinyo ya uasherati wa mwanamke huyu *{yaani, mafundisho yake ya uongo}.* Kwa vile Shetani ndiye ampaye mnyama nguvu zake, kiti chake cha enzi pamoja na uwezo mwingi ***{soma Ufunuo 13:2};*** basi ni wazi kwamba mwanamke huyu anatumia udanganyifu wake kuzifanya falme hizi kumnyenyekea *{amezikalia}.* Kwa kuwa tumemfahamu mwanamke; hebu sasa turudi katika pointi yetu tafadhalini. Ni nani mnyama huyu aliyekaliwa na mwanamke? Tuliona kwamba ufalme wa Rumi baada ya jeraha lake la mauti kupona, ulikuwa uendelee kwa kuinuka kwa falme *{pembe}* ndogo ndogo zenye kubeba jina na tamaduni zake. Na tukaona pia kwamba falme *{pembe}* tatu za kwanza kati ya kumi hazikuwa za Warumi, hivyo basi, hazikukubaliana na kanisa la Kirumi/Katoliki ***{soma Danieli 7:8},*** kwa hivyo kwa msaada wa mfalme wa mashariki mwa Rumi, kanisa hilo likawang'oa/likawaangusha.

Basi baada ya hapo, falme zote zilizosalia zilizoendelea kuinuka kuanzia kwa mfalme Justini katika mwaka wa 554 B.K. zilikubaliana na kanisa la Kirumi *{mwanamke}* na ziliapishwa na mkuu wa kanisa hilo *{yaani, Papa}* kushika mamlaka. Hii ina maana kwamba, zilitawala chini yake na hivyo zikaitwa kuwa falme zilizobarikiwa na kukubalika. Ukihesabu kuanzia kwa Justini *{pembe ya nne};* Charlemagne *{pembe ya tano};* Otto von *{pembe ya sita};* Charles V *{pembe ya saba};* Napoleoni *{pembe ya nane};* Hitla – Musolini *{pembe ya tisa};* utapata jumla ya pembe *{falme}* sita zilizoinuka zenye kujinyenyekeza chini ya kanisa la Kirumi na kuapishwa na Papa. Hii ndiyo maana ya kukaliwa na mwanamke.

Tunamaanisha nini hapa? Mnyama wa Ufunuo 17, ni ufalme wa Kirumi katika nyakati za kuinuka kwa pembe kumi. Pia ni wakati wa baada ya mwaka wa 325 B.K. pindi ambapo kanisa la Kirumi lilipoafikiana na mfalme Constantine na likaamka kwa nguvu. Kwa vile ndilo kanisa lililozing'oa zile pembe *{falme}* tatu za kwanza kuinuka; na ulikuwa ni wakati ambao vichwa vyote vya Ufunuo 13 vilianguka; basi lile lililosalia na kwendelea katika mfumo huo ni mwanamke huyo kuvikalia vichwa saba kati ya kumi katika Ufunuo 13. Ni hizi pembe saba zilizosalia za Danieli 7:7 na ambazo ndizo zile za Ufunuo 13, ndizo ambazo zinaitwa vichwa saba katika Ufunuo 17; ni zile zote zilizokuja katika kipindi cha kanisa hilo na kuapishwa nalo. Mungu anasema kwamba; ***"…Vile vichwa saba ni milima saba anayokalia mwanamke huyo. Navyo ni wafalme saba. Watano wamekwisha kuanguka, na mmoja yupo, na mwingine hajaja bado. Naye atakapokuja imempasa kukaa muda mchache. Na yule mnyama aliyekuwako naye***

***hayuko, yeye ndiye wa nane, naye ni mmoja wa wale saba, naye aenenda kwenye uharibifu" Ufunuo 17:9-11.***

Ili tuelewe vizuri unabii uliooneshwa hapo juu uhusuo Wafalme saba; basi ni sharti tuanzie kwa ***"mmoja aliyepo".*** Unabii wa Ufunuo 17 uliwekwa wazi kwa Kanisa kupitia kwa mjumbe ambaye Mungu alimtumia katika kulirejeza Kanisa lake juu ya msingi wa kweli. Katika mwaka wa 1929 B.K. mkuu wa Kanisa la Mungu duniani kote, alifundisha unabii kuhusu pembe ya tisa iliyokuwa ikitawala wakati huo. Ulikuwa ni wakati wa Hitla na Musolini. Hii ilikuwa ni pembe ya tisa kati ya kumi za Ufunuo 13, na ni kichwa cha sita kati ya saba katika Ufunuo 17. Ndiye aliyetajwa kwamba ***"mmoja yupo".*** Katika kipindi hicho; vitano kati ya vichwa saba vilikuwa vimekwisha anguka tayari; yaani kuanzia kwa Justini – mwaka wa 554 B.K; Charlemagne – mwaka wa 800 B.K; Otto – mwaka wa 962 B.K; Charles – mwaka wa 1520 B.K; na Napolioni – mwaka wa 1804 B.K; naam, watano hao walikuwa wamekwisha anguka tayari ***{soma Ufunuo 17:10}.***

Basi tangu kuanguka kwa muungano wa Hitla na Musolini mpaka sasa, hatujaona tena utawala mwingine wa Kirumi ukiinuka. Kwa hivyo basi; ***"mwingine hajaja bado",*** na ndiye tunayemtazamia. Yeye ni nani? Hivi sasa tunaona katika nchi za Ulaya, kuinuka kwa Jumuiya ama Muungano wa Ulaya ambao uko makini sana katika kusikiliza kile asemacho Papa. Naye Papa pia ana nguvu ya kujihusisha katika maswala ya kisiasa na kidini kote duniani. Hii ndiyo pembe ya kumi na ya mwisho ya Ufunuo 13, na ni kichwa cha saba katika ufunuo 17; na kwa habari zake, Bwana wetu anasema; ***"Naye atakapokuja imempasa kukaa muda mchache" Ufunuo 17:10.***

Sasa basi wapendwa; je! mnaona jinsi ambavyo unabii huu unavyoshabihiana kabisa na vipindi pamoja na matukio ya ulimwengu? Huu ni uthibitisho tosha kwamba ujumbe huu ni ujumbe wa Mungu mwenyewe.

## PEMBE KUMI ZA UFUNUO 17

Tumeona vyema habari za pembe kumi za Danieli 7:7 na Ufunuo 13. Lakini hapa tena tunaona habari za pembe nyingine kumi. Je! hizi zinatoka wapi? Katika Danieli 2, mfalme Nebukadreza alioneshwa ufalme wa nne ukiwa na vidole kumi, na aliambiwa kuwa hivyo vidole kumi ni wafalme kumi ambao watajaribu kuungana lakini kwa shida ***{soma Danieli 2:42-43}.*** Kwa vile huu ufalme wa nne wa Danieli 2 ndio ule ufalme wa nne wa Danieli 7, na ndiyo pembe ya kumi ya kile kichwa cha saba cha Ufunuo 17; na huku pia kipindi cha mwisho kilionekana kuwa kuwa na vidole kumi ***{soma Danieli 2:33};*** basi ni wazi na kweli kwamba hiki kichwa cha saba cha Ufunuo 17 *{yaani Muungano wa Ulaya}* kitakuwa na falme ndogo-ndogo kumi. Hivi vidole *{falme}* kumi ni tofauti na zile pembe kumi za Ufunuo 13; maana hivi vitatawala vyote kwa pamoja *{kwa wakati mmoja}* vikiwa vimesimama juu ya pembe ya mwisho. Naam; Bwana wetu anasema; ***"Na zile pembe kumi ulizoziona ni wafalme kumi, ambao hawajapokea ufalme***

***bado, lakini wapokea mamlaka kama wafalme muda wa saa moja pamoja na yule mnyama" Ufunuo 17:12.***

Pembe za Danieli 7, ambazo ndizo za Ufunuo 13; ziliinuka kwa kufuatana, moja baada ya nyingine. Bali hizi za Ufunuo 17, zinainuka zote kwa pamoja na kwa wakati mmoja. Na katika unabii huu, hapo ndipo mahali tulipo sisi leo. Naam; tuko katika vile vidole kumi vya ndoto ya Nebukadreza ambavyo pia ndizo pembe kumi za Ufunuo 17; zikija mara hii katika mfumo wa Muungano wa Ulaya ambao hivi punde tu utamchagua mfalme *{raisi}* mmoja awe juu yao wote ***{soma Ufunuo 17:13}***. Tuko katika sehemu ya mwisho kabisa ya huu mfumo wa Kibabeli. Mara baada ya huu Muungano wa Ulaya kusimama; na wakati ukiendelea kutawala; basi ***"…katika siku za wafalme hao*** *{hivyo vidole kumi}* ***Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaangamizwa milele, wala watu wengine hawataachiwa enzi yake; bali utavunja falme hizi zote vipande vipande na kuziharibu, nao utasimama milele na milele" Danieli 2:44.*** *{Kwa habari za kina zaidi kuhusu huo ufalme wa Mungu; agiza kitabu chetu kisemacho,* ***"UFALME WA MBINGUNI",*** *ili ujifunze zaidi; utatumiwa bure kitabu hicho pasipo malipo}.*

## MNYAMA NI UFALME WA KISHETANI

Tayari tumeelewa vizuri kwamba mnyama ni mfalme ama ufalme. Na tumeelewa vizuri pia kwamba mnyama wa Ufunuo 13 ni mkusanyiko wa falme. Tumeelewa pia kwamba Yohana aliishi katika siku za ufalme wa Rumi ambao ndio kile kichwa kilichopata jeraha la mauti. Na kwamba baada ya jeraha la mauti, ufalme huo ukaendelea kwa mfululizo wa kuinuka kwa falme ndogo ziitwazo pembe. Na kwa wakati huu, tunangojea kuinuka kwa pembe ya mwisho ambayo hivi sasa inaanza kuchukua mahala pake kwa jina la Muungano wa Ulaya. Mara Muungano huo wa Ulaya utakapowekwa chini ya mfalme *{raisi}* mmoja; basi utakuwa ndiyo yule mnyama ambaye tunaonywa dhidi yake kwamba tusipokee alama yake, wala nambari yake, wala kuiabudu sanamu yake. Sasa je! ni nini sanamu, alama na nambari ya mnyama huyu *{Muungano wa Ulaya},* ambaye ni pembe ya mwisho ya ufalme mtakatifu wa Rumi?

Kamwe huwezi kujiepusha na kitu usichokijua. Kwa hivyo basi; ni muhimu sana kuhakikisha kwamba tunayafahamu mambo haya. Ni kwa nini ufalme wa Rumi unaitwa **"Ufalme Mtakatifu wa Rumi?"** Wasomaji wengi wa biblia hufikiri kwamba; jina hili **"Ufalme Mtakatifu wa Kirumi"** lilitokana na ufalme huo kumwabudu Mungu wa mbinguni ambaye peke yake ndiye Mtakatifu. Lakini tunaporudi kwa Mungu, yeye anatuambia kwamba ufalme huo unamwabudu Shetani; maana anasema, ***"…yule joka*** *{yaani, Shetani}* ***akampa*** *{mnyama ama ufalme}* ***nguvu zake na kiti chake cha enzi na uwezo mwingi" Ufunuo 13:2.*** Hii ina maana kwamba; hizi falme nne zote, zimejengwa juu ya msingi wa Shetani, na zikiabudu pia miungu ya sanamu ***{soma Yeremia 2:11; 10:1-5}.***

Hebu tuyadhibitishe haya kwa maandiko tafadhalini. Mfalme Nebukadreza aliabudu mungu aliye mpinzani *{kinyume}* wa Mungu wa mbinguni ambaye ni Mungu wa Danieli,

Shadraka, Meshaki na Abednego ***{soma Danieli 3:12}.*** Mfalme Dario wa Umedi na Uajemi naye aliabudu miungu ya kipagani *{yaani, sanamu}* iliyo kinyume na Mungu wa mbinguni wa akina Danieli ***{soma Danieli 6:5,7-9,16}.*** Ufalme wa Uyunani *{Ugiriki}* uliyoongozwa na Alekzanda mkuu pia uliabudu miungu iliyo kinyume na Mungu wa mbinguni ***{soma Matendo 17:18-19; 19:28}.*** Kadhalika ufalme wa Warumi pia ambao ndiyo huyu mnyama tunayemzungumzia hivi sasa waliabudu miungu ya kipagani *{sanamu}* iliyo kinyume na Mungu wa mbinguni; naam; waliabudu mungu jua, Ishita *{waliyemwita malkia wa mbinguni}* n.k.

Na kwa hivyo basi; ushahidi huu wote wa maandiko unathibitisha wazi kwamba, mfumo mzima wa mnyama huyu ni wa Kishetani *{yule joka; soma **Ufunuo 12:9**};* maana ni yeye Shetani ndiye atendaye mambo kinyume na kumpinga Mungu wa mbinguni, na ndiye awafundishaye wanadamu kufanya kama yeye. Kwa sababu hiyo basi; huu ufalme wa Warumi unapojiita kuwa ni **"Ufalme Mtakatifu wa Kirumi",** unajiita kutokana na hiyo miungu yao, na wala si Mungu wa mbinguni. Hii ina maana kwamba; cho chote kile kitokanacho na ufalme huo, kinatokana na mungu wa dunia hii, yaani, Shetani ***{soma 2 Wakorintho 4:4; Yohana 14:30; Waefeso 2:2}.*** Basi hali tukiyaelewa haya; hebu sasa turudi katika mada yetu.

## SANAMU YA MNYAMA

Sanamu ya kitu ni mfano halisi ama mwonekano wa nje wa kitu hicho. Sanamu yawezakuwa picha, ama iliyojengwa, ya kuchongwa n.k. Na kwa hivyo kila aitazamaye ataelewa moja kwa moja kuwa ni sanamu ya nini ama ya nani. Basi vivyo hivyo; kwa vile mnyama ni ufalme, na ufalme huo ni ule wa Warumi ambao unaendelea kuinuka huko ulaya kwa jina la Muungano wa Ulaya; sanamu yake ni lazima iwe mfano wa huo ufalme, inayofuata sheria za ufalme huo na hata mila , desturi na tamaduni zake. Sasa je! ni muungano gani ulioanza kwa mfano wa ufalme wa Warumi na unaofuata mila, desturi na tamaduni zake?

## MNYAMA MWENYE PEMBE MBILI

***"Kisha nikaona mnyama mwingine, akipanda juu kutoka katika nchi; naye alikuwa na pembe mbili mfano wa Mwana-kondoo, akanena kama joka" Ufunuo 13:11.***

Kumbukeni kwamba mnyama ni mfalme ama ufalme. Na pia tunafahamu kwamba katika biblia, Mwana-kondoo humwashiria Yesu Kristo ***{soma Ufunuo 5:6; Yohana 1:29}.*** Vile vile tunafahamu pia kwamba katika biblia, joka humwashiria Shetani ***{soma Ufunuo 12:9}.*** Kwa hivyo mnyama *{ufalme}* huyu ana falme *{pembe}* mbili ndogo zenye kufanana na Kristo *{Mwana-kondoo},* lakini zinanena kama Shetani *{joka}.*

Sasa basi; Shetani huongeaje? ***“Yule ambaye kuja kwake ni kwa mfano wa kutenda kwake Shetani, kwa uwezo wote, na ishara na ajabu za uongo…yule mpingamizi, ajiinuaye nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu ama kuabudiwa; hata yeye mwenyewe kuketi katika hekalu la Mungu, akijionyesha nafsi yake kana kwamba yeye ndiye Mungu” 2 Wathesalonike 2:9,4;*** soma pia ***Mwanzo 3:4-5.*** Tunachosema hapa ni kwamba; Shetani hunena kwa kumpinga Mungu katika kila jambo asemalo.

Naam, wapendwa; ni ufalme *{muungano}* gani duniani leo unaofuata mambo ya ufalme wa Kirumi *{sanamu},* wenye falme mbili ndogo, na wenye kujionesha kumwashiria Kristo, na huku pia ukinena kama Shetani *{kwa kupingana na biblia}?* Twende pamoja tafadhali.

***“Naye atumia uwezo wote wa mnyama yule wa kwanza mbele yake. Naye aifanya dunia na wote wakaao ndani yake wamsujudie mnyama wa kwanza, ambaye jeraha lake la mauti lilipona. Naye afanya ishara kubwa, hata kufanya moto kushuka kutoka mbinguni uje juu ya nchi mbele ya wanadamu. Naye awakosesha wale wakaao juu ya nchi, kwa ishara zile alizopewa kuzifanya mbele ya huyo mnyama, akiwaambia wakaao juu ya nchi kumfanyia sanamu yule mnyama, aliyekuwa na jeraha la upanga naye akaishi” Ufunuo 13:12-14.***

Kama mnakumbuka; tuliona pembe ndogo ***{Danieli 7:8}*** ikiinuka na kutumia uwezo wa mfalme wa mashariki wa Warumi *{mnyama}* kuzing’oa pembe *{falme}* tatu za kwanza kuinuka kati ya kumi. Tukaona pia ukibadili nyakati na sheria za Mungu na kuwadhoofisha watakatifu wake *{yaani, Kanisa la Mungu;* ***Danieli 7:25****}.* Iliyafanya haya yote kwa kutumia mamlaka na tamaduni za Wafalme wa utawala wa Warumi *{mnyama wa kwanza}.* Na jambo hili ni la kweli na liko wazi kabisa; maana Warumi walibadili nyakati *{ama majira}.* Badala ya siku kuanza jioni hadi jioni nyingine kulingana na mpango wa Mungu ***{soma Mwanzo 1:13,15; Walawi 23:32};*** walianzisha utaratibu wao wa siku kuanzia saa sita usiku hadi saa sita usiku mwingine; kwa hivyo wakayabadili majira *{nyakati}.* Tena badala ya kumwabudu Mungu wa mbinguni katika siku yake takatifu ya ibada aliyoagiza *{yaani, siku ya saba ya juma ambayo ni Sabato};* waliifuata miungu yao ya kipagani; wakamwabudu mungu jua katika siku ya kwanza ya juma *{jumapili}* na kuiita siku hiyo kufuatia jina la huyo mungu wao jua *{yaani, Sun-day; maana yake ni Siku ya jua}.* Wakati hii pembe ndogo ilipoinuka kwa nguvu; iliyasimamia haya matendo yote ya kipagani ya ufalme wa Rumi na kuanza kuyafundisha kama mafundisho ya Kristo. Kwa kuwa tumefahamu vyema kwamba hii pembe ndogo ni Kanisa la Kirumi *{Katoliki};* basi ni wazi pia kwamba ndilo linalooneshwa hapa kama mnyama mwenye pembe mbili.

Hebu na tupate uthibitisho zaidi. Kila mtu anayefuatilia maswala ya dunia leo anafahamu vyema kwamba Kanisa la Rumi *{Katoliki}* lina mfumo wa utawala uliogawanyika pande mbili. Vatikani ni serikali kamili ya kidunia yenye mabalozi *{wawakilishi}* wake kote duniani. Pia ina serikali ya Kikanisa yenye wawakilishi wake kote duniani. Serikali zote hizi mbili ziko chini ya kiongozi mmoja *{yaani Papa}* ambaye ni mkuu wa Kanisa la Kirumi, anayejiita kuwa ni mwakilishi wa Yesu Kristo duniani. Kwa hivyo, hii serikali ya kidunia pamoja na hii ya kikanisa ndizo pembe mbili za mnyama huyu. Tamaduni na mafundisho ya Vatikani ni yale yote ya

ufalme wa Rumi *{mnyama wa kwanza},* na mfumo wa utawala wake na utendaji wake duniani ni ule ule wa utawala wa Kirumi. Hebu na tuelewe kwa uwazi zaidi.

Tunahitaji kuthibitisha kwamba pembe ndogo ya Danieli 7:8 ndiye mnyama mwenye pembe mbili. Pembe ndogo inanena kinyume na Mungu *{inampinga}* na kuwapiga vita watakatifu wa Mungu aliye juu *{soma Danieli 7:25}.* Kadhalika mnyama mwenye pembe mbili pia ananena kinyume na Mungu *{anampinga}* na kupigana na watakatifu wake ***{soma Ufunuo 13:12,14-15}.*** Pembe ndogo inainuka kutoka katika ufalme wa Rumi ***{Danieli 7:8}.*** Kadhalika mnyama mwenye pembe mbili anainuka kutoka katika ufalme wa Rumi na kuufuata ***{Ufunuo 13:12-14}.*** Sasa basi; ni jambo gani lililo wazi zaidi ya hili? Hii pembe ndogo ambayo tumethibitisha kuwa ndiye mnyama mwenye pembe mbili, pia ndiye nabii wa uongo! Tutajuaje? Hebu basi tulithibitishe hili nalo.

Mnyama mwenye pembe mbili aonesha ishara, hata kufanya moto kushuka kutoka mbinguni; anadanganya watu ***{soma Ufunuo 13:13}.*** Kadhalika pia nabii wa uongo anayafanya hayo hayo ***{soma 2 Wathesalonike 2:9; Ufunuo 19:20}.*** Mnyama mwenye pembe mbili anafanya maajabu *{ishara}* yake mbele ya mnyama ***{soma Ufunuo 13:14}.*** Kadhalika nabii wa uongo anafanya maajabu *{ishara}* yake mbele ya mnyama ***{soma Ufunuo 19:20}.*** Kwa hivyo, hawa wawili ni mmoja na ni kitu kile kile!

Lakini pia; jueni na fahamuni kwamba, hii pembe ndogo, ambayo ni mnyama mwenye pembe mbili, na ambaye sasa tumethibitisha kuwa ndiye nabii wa uongo; yeye ndiye yule kahaba *{mwanamke aketiye juu ya mnyama}* wa Ufunuo 17. Na hii ni kwa sababu; kahaba huyu amejengwa juu ya mnyama ***{soma Ufunuo17:3},*** naye pia anafanya vita dhidi ya watakatifu na kulewa kwa damu yao ***{soma Ufunuo 17:6}.*** Tena kahaba huyu ananena kinyume na Mungu *{anampinga; **Ufunuo 17:4**}.*

Basi kwa kuwa hii pembe ndogo ndiyo mnyama mwenye pembe mbili, nabii wa uongo ambaye pia ni mwanamke kahaba, mwenye kutumia tamaduni na mafundisho yote kutoka kwa mnyama wa kwanza *{ufalme wa Rumi};* naam, yeye ndiye sanamu ya mnyama! Akijifanya kuuunganisha ulimwengu wote kuwa chini ya Kristo *{Mwana-kondoo},* anawadanganya watu waunde jumuiya moja ya dunia yote inayofuata mila, desturi na tamaduni zote za Kirumi *{kama joka}.* Na hivyo, watu watakubali; wakidhani kuwa wameunganishwa katika kanisa, na kwa njia hiyo wataunda utawala wa dunia yote ulio sawa na ufalme wa Rumi *{sanamu; **Ufunuo 13:14**}.* Kanisa hili la Kirumi pia litautumia ufalme huo wa Rumi utakaoinuka kupigana na kuwatesa wale wote ambao hawataungana na jumuiya/muungano huo *{wasioabudu sanamu}.*

Huku wakijionesha kumwakilisha Kristo *{wakimweshimu kwa midomo yao},* lakini kwa mioyo yao wako mbali sana naye, kwa sababu wanafundisha mafundisho ya wanadamu badala ya sheria za Mungu ***{Marko 7:9};*** na kwa kunena kama joka, watawadanganya watu kuwafuata na hivyo kuabudu sanamu ya mnyama. Naye huyu kahaba amezaa makahaba, ambao ni makanisa yale yanayoonesha kujitenga naye huku yakiendelea kufuata mafundisho yake yaliyo

ya wanadamu. Naam; yeye ni **"MAMA WA MAKAHABA",** ***soma Ufunuo 17:5.*** Kwa hivyo hao makahaba wote waliozaliwa naye pia ni sehemu ya hiyo sanamu ya mnyama. Na sasa je! rafiki; utamfuata Mungu na kutii sheria zake ambazo ndizo pekee zitakazokufanya kutojiunga na jumuiya hiyo; ama utawafuata wanadamu katika jumuiya hiyo na hivyo kuiabudu sanamu ya mnyama? Uamuzi ni wako; chagua mwenyewe!

## ALAMA YA MNYAMA

Kutokana na maelezo hayo hapo juu yahusuyo sanamu ya mnyama; basi tunaamini kuwa ni rahisi zaidi sasa kuelewa alama na nambari yake. Kwa nini? Kwa sababu tayari tumejua kwamba mnyama huyu ni ufalme wa Rumi unaoinukwa kwa jina la Muungano wa Ulaya. Sasa je! ni alama gani ya ufalme wa Rumi ambayo huo Muungano wa Ulaya utaiweka katika vipaji vya nyuso zao na katika mikono yao ya kuume *{ama kulia}*? Hebu na tufuatilie maandiko katika kulifahamu jambo hili pia.

*{1} Alama hii ni kitu watakachotiwa watu katika vipaji vya nyuso zao na katika mikono yao ya kuume* ***{soma Ufunuo 13:16}.***

*{2} Alama hii ni kitu ambacho wote watakaokipokea watakinywea kikombe cha ghadhabu {hasira} ya Mungu* ***{soma Ufunuo 14:9-10}.***

*{3} Alama hii ni kitu ambacho wote watakaokikataa watateswa na hata kuuawa na mawakili wa Shetani* ***{soma Ufunuo 13:15-17}***

Sasa je! alama hii ni kitu gani hasa? Maana kuipokea alama hii kutamkasirisha Mungu; na kadhalika pia kutoipokea kutamkasirisha Shetani! Je! hiki ni kitu gani hasa? Ghadhabu ya Mungu huwaangukia wale wote wasiomtii ***{soma Wakolosai 3:5-6}.*** Hali kadhalika; ghadhabu ya Shetani pia huwaangukia wale wote wazishikao *{wanaozitii}* amri za Mungu na imani ya Yesu Kristo ***{soma Ufunuo 12:17}.*** Kwa hivyo basi; ni wazi kwamba hii alama ya ufalme wa Rumi *{Muungano wa Ulaya}* ni kitu ambacho kukipokea kutamfanya mtu kutotii *{kuvunja}* sheria za Mungu. Vile vile ni kitu ambacho kukikataa kutamfanya mtu kutii sheria za Mungu.

Sasa basi; ni kitu gani hasa ambacho ufalme wa Rumi ulikianzisha, ambacho mtu akikifuata anavunja amri ya Mungu, na ambacho ni alama ya ufalme huo? Ili kukielewa vizuri zaidi; basi tunahitaji kwanza kuielewa alama ya Mungu ambayo pia hutiwa katika vipaji vya nyuso na katika mikono ya kuume.

Mungu aliagiza akisema; ***"Yafunge*** *{maagizo ya Mungu/sheria}* ***yawe dalili juu ya mkono wako, nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yako*** *{katika paji la uso}****" Torati 6:8;*** *soma pia* ***11:8.*** Je! rafiki, umeanza kupata mwanga wa ufahamu? Alama hii ni ya kiroho, na wala si kitu cha kimwili kinachoonekana katika nyuso ama mikono ya watu! Sasa basi; kama ilivyo kwamba, sheria za Mungu ni alama iliyo katika vipaji vya nyuso na katika mikono ya

kuume ya wote wazishikao; kadhalika hii alama ya ufalme wa Rumi *{mnyama}* ni sheria! Kutiwa katika kipaji cha uso, kuna maana ya kuzikubali akilini ama moyoni; na kutiwa katika mkono wa kuume, kuna maana ya kuzitenda ama kuzishika *{kuishi kwazo}*. Katika sheria za Mungu; ipo amri ya nne ambayo Mungu anaiita kuwa ni alama ya ufalme wake. Anasema; ***"Basi mtaishika hiyo Sabato; kwa kuwa ni takatifu kwenu…Ni ishara** {alama}* ***kati ya mimi na wana wa Israeli milele…", soma Kutoka 31:14,16-17.***

Kinyume na sheria za Mungu, na katika kuabudu mungu wao wa kipagani jua; ufalme wa Kirumi uliikataa Sabato Takatifu ya Mungu *{ambayo ni alama yake},* na wakaanzisha siku yao ya ibada kufuatia jina la huyo mungu wao jua, wakaiita **"Siku ya jua"** *{yaani, Sun-day}* kama alama ya mungu wao, na ya ufalme wao. Wakati mfalme Constantine alipoukubali Ukatoliki, yeye pia aliamuru kwamba siku ya mungu wao jua iwe ndiyo siku ya ibada, na wakaanza kuwatesa wale walioitunza Sabato ya Mungu wa mbinguni. Kwa hivyo, hii siku ya mungu jua {yaani Jumapili} ndiyo alama ya mnyama, ambayo kuitii ni kutokutii Sabato ya Mungu. Naam; ukiipokea alama ya mnyama ambayo ni utunzaji wa Jumapili kama siku ya ibada, utakuwa umemkaidi Mungu kwa kuvunja Sabato yake. Kadhalika; ukiitunza Sabato ambayo ni alama ya Mungu; utakuwa umemkaidi mnyama kwa kutotii Jumapili yake; na kwa sababu hiyo, mnyama mwenye pembe mbili *{Kanisa la Kirumi}* atakufanya uteswe na hata kuuawa na mnyama wa kwanza *{yaani, ufalme wa Rumi; soma **Ufunuo 13:15**}.* Kumbukeni kwamba; haya maneno ni maneno ya kweli ya Mungu wa mbinguni asiyesema uongo kamwe. Ni hivi punde tu tutayashuhudia mambo haya yakitimia mbele ya macho yetu kwa kutimizwa na huo Muungano wa Ulaya kwa kushirikiana na Kanisa la Kirumi. Sasa je! mpendwa; wewe tayari umeishapokea alama ya mnyama ambayo ni utunzaji wa Jumapili kama siku ya ibada? Bado unayo nafasi ya kufanya mabadiliko na kuamua kumtii Mungu *{agiza kitabu chetu kisemacho **"AMRI KUMI",** ili ujifunze zaidi yakupasayo kufanya, tutakutumia bure bila malipo}.*

## NAMBARI YA MNYAMA

Zaidi ya sanamu ya mnyama *{muungano wa dunia yote kwa njia ya kanisa},* na alama *{siku ya ibada ya ufalme},* ufalme wa Rumi utaamuru kwamba, ***"…mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa ile, yaani, jina la mnyama yule, au hesabu ya jina lake" Ufunuo 13:17.*** Basi, ***"Hapa ndipo penye hekima. Yeye aliye na akili {soma Zaburi 111:10}, na aihesabu hesabu ya mnyama huyo; maana ni hesabu ya kibinadamu. Na hesabu yake ni mia sita, sitini na sita" Ufunuo 13:18.*** Sasa basi; hii nambari **666** ni nini na ina maana gani hasa? Kwanza tumeambiwa kwamba hii nambari ni sawa na jina la mnyama, na tunafahamu kwamba jina la mnyama ni ufalme wa Rumi. Kwa hivyo; kupokea nambari hii ni kukubali kuwa Mrumi kwa njia ya kuzikubali sheria na tamaduni zake *{katika paji la uso wako}* na kuishi kwazo *{kutiwa katika mkono wako wa kuume},* naam; kuishi kwa mfumo wa maisha ya Kirumi.

Ufalme ni wa Rumi *{mnyama}.* Kwa hivyo, ukikubali kuishi kama Warumi, kwa kukubali mafundisho yao ya udanganyifu yanayofundishwa na kanisa lao, basi wewe pia utakuwa Mrumi mwenye kubeba jina la ufalme huo ambalo pia ni nambari yake. Sasa basi, ni kwa jinsi gani jina **ROMAN** tafsiri yake ni **666**; maana nambari ndilo jina la mnyama? Hili jina ROMAN limefasiriwa kutoka katika jina la Kigiriki "**AATEINOC** *{Lateinos}*" lenye maana ya Mlatini *{Latin man}.* Katika nambari za Kigiriki herufi hufuata kwa naman hii:-

**A {L} – 30**

**A {A} – 1**

**T {T} – 300**

**E {E} – 5**

**I {I} – 10**

**N {N} – 50**

**O {O} – 70**

**E {E} – 200**

**JUMLA YAKE NI 666.**

*{Hapa ni kwa herufi za Kigiriki na si Kiingereza}.*

Kwa hivyo wapendwa; fahamuni jambo hili tafadhalini kwamba; kufuata mila, desturi, tamaduni na sheria za huo ufalme *{mnyama},* basi huko ndiko kuwa na nambari ya mnyama! Endapo mtu wa kabila lo lote lile atakujia akiwa amevalia mavazi ya Kimasai na huku pia akizungumza lugha ya Kimasai; basi moja kwa moja utasema kwamba mtu huyo ni Mmasai. Kadhalika mtu ye yote atakayechukua mfumo wa maisha ya Warumi na kuishi kwa mfumo huo hata kama ni kwa njia *{mafundisho}* ya kanisa; basi moja kwa moja mtu huyo atakuwa Mrumi, mwenye kubeba jina la mnyama ambalo ni nambari yake.

Mambo mengi wayafanyayo watu ulimwenguni leo, msingi wake ni mila, desturi na tamaduni za Warumi. Kuanzia katika kuhesabu masaa, siku, miezi, miaka; maadhimisho ya sikukuu, na njia *{namna}* za kuabudu; naam, kuadhimisha vitu kama Krismasi, Pasaka iitwayo Ista, Mwaka mpya, Siku ya wapendanao *{Valentines}* na kadha wa kadha *{agiza ujumbe wetu usemao **"ROHO YA SIKUKUU ZA BWANA"** , kwa maelezo mengine ya msaada zaidi; tutakutumia bure ujumbe huo}.* Haya yote ni mambo ya Warumi yanayomfanya ye yote mwenye kuyafuata kuwa Mrumi. Kwa kuishi kwayo, umeyakubali akilini mwako *{ambako ni kutiwa chapa katika paji la uso wako}* na kuyatenda kwa mwenendo wako *{ambako pia ni kuwa na chapa hiyo katika mkono wako wa kuume}.* Na hivyo basi; unakuwa na nambari **666.**

Na sasa basi wapendwa; kupitia kwa ujumbe huu, Mungu wa mbinguni anawaita akisema; ***"Tokeni kwake, enyi watu wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake…Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami. Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi, kama mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha enzi" Ufunuo 18:4; 3:20-21.*** Basi kama vile Kristo alivyorudia kusema mara kadhaa; ni wale tu walio na hekima na ufahamu ***{soma Mathayo 13:11, Mithali 1:7; Zaburi 111:10}*** ndio watakaolielewa jambo hili ***{soma Ufunuo 13:18; 17:9}.*** Sasa je! wewe ni mmoja wa hao wenye hekima na ufahamu? Basi mwenye masikio na asikie!

Wapendwa; Kanisa la Mungu la kweli alilolianzisha Yesu Kristo mwenyewe, liko hapa hivi sasa kwa ajili yako. Kwa hivyo basi; endapo utapenda kujifunza mengi zaidi kuhusu kweli halisi za Biblia; tunavyo vitabu na majarida mengi yenye mada *{masomo}* mbali mbali yanayoweka wazi ukweli wa Biblia. Na ifahamike kwamba; mafundisho yetu yote ni Biblia imesema, na kamwe hatufundishi mafundisho ya kimadhehebu ya kidini wala mapokeo ya wanadamu. Tena, vitabu na majarida yetu yote yanatolewa bure kwa ye yote atakaye pasipo malipo. Uliza swali ama mada yo yote ile ya biblia, na tutakutumia kitabu ama jarida lenye majibu sahihi ya biblia bure.

***Wasiliana nasi kwa anuani zifuatazo:-***

***KANISA LA MUNGU – TANZANIA***

***Nambari za simu; +255 753 359 179, +255 688 359 179 na +255 655 659 179.***

***Barua pepe; Ukweliwabiblia@yahoo.com.sg***

***NA***

***KANISA LA MUNGU – KENYE***

***Barua pepe; endcog@gmail.com***

***Neema na iwe kwenu, na amani zitokazo kwa Mungu Baba yetu, na kwa Bwana wetu Yesu Kristo. Utukufu una yeye tangu milele, sasa na hata milele; Amina.***